https://dspace.org/

# Mayelezo Maae Kuhusu ‘Vita’ Kama Ilivokuja Katika Makala ya ‘Yatokanayo Na Mkaza’: Gombo La Isimu Tumi Ni Kufuwata Sat I Za Majagina Wa Isimu

**Karama, Mohamed**

**2024-01**
http://ir-library.kabianga.ac.ke/handle/123456789/741

Downloaded from a DSpace repository. https://dspace.org/

## Mayelezo Mačače Kuhusu 'Vita' Kama Ilivokuja Katika Makala ya 'Yatokanayo Na Mkaza'

Hivi majuzi Maalim Abḍilaṭif Abḍalla (2024) aliyenreleza ufafanuzi wake kuhusu neno 'mkaza', makala yaliyosambazwa ḳenye mtanrawo wa kijamii; nami piya alinileteya nakala hiyo kikašani ṁangu, namšukuru ḳa hisani hiyo. Bila ya kuregeleya yaliyoelezwa katika makala haya ya Mkaza, awali Maalim alisibu ḳa kutufunuliya kuwa asili ya 'vita' ni 'kita'; ḳamba yaṭokana na /ki-ta/ na ikawa /ki-/ ni kiyambiši ča ngeli na /-ta/ ni kitenzi čake (Abḍalla [2017] akinukuliwa katika ḍaka la Kina Wenyewe, 2017)[1]. Mreješo wetu huu uṭahusu asili na fasili aliyoyeleza Maalim kuhusu 'vita' na 'kita' lakini niṭačanganuwa kiisimu na maoni yangu yaṭakuwa ṭafauṭi na yake.

Kwa kutumiya Ṭaraṭibu ya Ulinganiši na mapisi yaliyoko baina ya luğa zilizosampuliwa na kiSwahili nripo tulipočota na kučanganuwa data yetu. Tumečaguwa sampuli ya luğa 'kuu' za mabara mane: Afrika, Ulaya, Asiya, Amerika Kusini kwa sababu luğa hizo zili(na)ṭagusana na kiSwahili kwa ukuruba (kimasafa) au sababu za kiyučumi, kijamii, au, kisiyasa. Ṫaafiki peṇḍekezo kuwa mṭagusano huu wa luğa ainaṭi husababiša ukopano na ṫahiṭimiša kuwa asili ya neno 'vita' ni la kukoṗa kuṭoka kiPorṭugesi kuja kiSwahili paṁe kuliṭokeya uvumbuzi ili kulipa muunro wa mofolojiya ya kiSwahili. Luğa ni nyingi sana katika mabara haya lakini tuličaguwa kimakusudi luğa fulani kwa sababu tulifahamu zaṭošeleza kupata data tuliyohiṭajiya kwa učanganuzi na mafafanuzi yetu.

**Usuli wa 'kita'**

Kisisi, 'vita' ni neno lililokoṗa kuṭoka luğa za kiRomansi (kiFaransa, kiṬaliyani, kiHispanyola, kiPorṭugesi) au kiJarumani (ḳa mbali sana kisauṭi) kama jeḍwali linavoaširiya hapa čini. Haswa, 'vita' ni kiPorṭugesi ḳa kubaḍilika /geha/ ikawa /kita/ ḳa kiSwahili. Ḳamba sauṭi /g/ ḳa kiSwahili huweza kuṭamḳa /k/ kama ḳenye neno /giza/, /kiza/. Ama /t/ huweza kugeuka /h/ kama ilivo katika kiMijikenra čoṭʰe. Ḳa mfano, /muhi/, /muho/ ni /mti/, /mto/ kiMijikenra na kiSwahili mṭawaliya. Ḳa hivo, /geha/ kiPorṭugesi ni /kita/ kiSwahili kwa sababu kiSwahili kina neno lake halisi la vita, kama tuṭakavoleza baaḍaye.

**Vita haigawiki**

Ufafanuzi wa kugawa /kita, vita/ haukuṭajwa katika makala ya Mkaza, Maalim aliuṭaja ḳenye makala tulorejeleya ṭanbihini, na tukitizama kiMijikenra kunawo mfano wa /čiṭsaka/ umoja na /viṭsaka/ wingi, ḳa maana ya 'kičaka/vičaka' *bush*/*bushes* na viyambiši ngeli ni /č/, /vi/. Ṭafauṭi na kiSwahili ambapo lazima palikuwako na umoja /kita/ kama alivosema Maalim, kwa sababu shariya ya kisarufi haikubali kuwako wingi bila umoja (Mazrui, 1981), kiMijikenra ambako neno /viha/ liko hakuna umoja wake /kiha/ au /čiha/ (nimeṭegemeya *Kamusi la Mgombato*, sikuuliziya kwa waṭaalamu). Na ikiwa hamuna umoja wa 'viha', na 'kita' inadhaniwa kuadimika kimatumizi, ṫasubutu kusema mfano huu wa kita/vita ni kama wa kiṭabu/viṭabu katika kiSwahili. kiSwahili kilivumbuwa wingi wa /kiṭabu/ ḳa kaiḍa ya upatanišo lakini /ki-/ katika /kiṭabu/ si mofimu tegemezi bali ni asili katika mofimu huru lililoṭoka kiyArabu /kiṭaab/ mzizi wake 'kṭb'. Hivo basi, ile /ki-/ katika neno /kita/ si kiyambiši ča ngeli bali huṭamḳa kama mofimu huru 'kita' ambayo iṭaruḍi ḳa kiPorṭugesi kama tulivosema awali. Mfano ṁengine ni neno 'vitamini' ambapo /vi-/ katika neno hilo ni silabi ya mofimu huru (nomino) na wala si kiyambiši ča ngeli wingi.

[1] Rejeleya ḍaka https://kinawenyewe.wordpress.com/2017/02/16/ni-kiasi-cha-sio-kiasi-ya/

**Je, /-ta/ ni ‘vita’?**

Ama kuhusu /-ta/, kama alivošahaḍiza Maalim k̇enye makala kaḍimu ya 2017 yaliyoeleza asili ya ‘vita’, k̇amba imetumika katika ‘humta pembe’ (ubeṭi wa 14 katika Utenzi wa Al Inkishafi) tuṭaona kuwa ina maana ya ‘kupiga’ kama ilivo katika Uṭeṇḍi wa Paṭe, ‘wawapi wata ziyemba? Mauṭi imewakumba’ (Sacleux, 1939 uk. 851) na imekuja k̇a maana ya ‘piga’ na piya kinahau ‘kupiga kilemba’. Ubeṭi wa 14 uliyorejelewa awali wasema hivi:

> Ni kama kisima kisicho ombe
> Chenye **mta** paa mwana wa ng’ombe
> Endao kwegema **humta pembe** (msisitizo ni wetu)
> Asipate kamwe kunwa maiye

Ḍuniya imefananišwa na kisima kisičo na kina na čalinrwa na ṁana wa ng’ombe ambaye humpiga pembe anayekikaribiya. Neno /m-ta/ na /hu-m-ta/ limetumika k̇a maana ya ‘kupiga’ katika ubeṭi huwo. Peṇḍekezo letu ni k̇amba /hu-m-ta/ na /wa-ta/ hiyo /-ta/ kama ilivo katika maneno hayo inaswilihi zaiḍi ‘kupiga’ kuliko ‘vita’ na mbali kiḍogo na ‘kušambulia’ kama ilivofasiliwa katika *Tenzi Tatu za Kale* (Mulokozi, 1999 uk. 85).

**čiSwahili činačo neno lake la ‘vita’**

Je, čiSwahili hačina neno limaanišalo ‘war’? Iṭaonekana činačo. ‘Kʰonro’ nrilo neno lenyewe. Na kama jeḍwali liyonešavo luğa za kiBantu: kiŠona, čiČewa, čiMidzičenra zinazo neno hilo hilo k̇a maṭamši ṭafauṭi ya čiSwahili: /kondo/, /nkhondo/, /kondo/ mṭawaliya. Neno hili ‘kʰonro’ limetumika k̇enye ubeṭi wa 68 katika Utenzi wa Al Inkishafi (Mlamali, 1980 uk. 60) nawo wasema hivi:

> Tafakari siku ya kwima **kondo** (msisitizo ni wetu)
> Ya kuaridhiwa kula kitendo
> Pindi madhulumu atapo ondo
> Achamba: Ya Rabbi namuwa naye.

Ṁanadamu anakumbušwa siku ya kusimama vita (Siku ya Kiyama) wakaṭi aloďulumiwa aṭakapo piga goti mbele ya Mungu aṁambiye aṁamuliye haki baina yake na alomďulumu. K̇a hivo čiSwahili činačo istilahi ya ‘vita’ ṭangu azali ikikumbuk̇a kuwa Uṭeṇḍi huu ulituṅġa k̇a luğa ya kiNgozi, mame-luğa wa kiSwahili.

**Ni sawa piya kusema ‘vita ya’**

K̇a minṭarafu ya mayelezo hayo juu, ni wazi basi, wasemawo ‘vita ya’ na ‘vita va’ wako sawa kisarufi na ni kiSwahili fasaha. Asemaye ‘vita va’ nrivo ilivo k̇a sababu kiSwahili ni luğa ya upatanišo wa kisarufi. Na asemaye ‘vita ya’ piya ni sawa k̇a sababu maneno yaliyokop̣a kuṭoka luğa nyengine katika kiSwahili huwek̇a k̇enye ngeli ya N-N (*Modern Swahili Grammar* (Mohamed, 2001)) ambayo mofimu kihusiši ni ‘ya’. K̇a mfano kiumoja ‘gari ya’, ‘kompyuta ya’, ‘ḍawa ya’, ‘vita ya’ na ‘gari za’, ‘kompyuta za’, ‘ḍawa za’, ‘vita za’ katika wingi. Ṭaweza piya kusema, “vitamini ya/za kujenga ṁili”, k̇a sababu hapa /vi-/ ni sehemu ya mofimu huru (nomino) na wala si kiyambiši ča wingi.

Ama kuhusu masiyala ya ‘vita ya’ kuwamo k̇enye ngeli mbili, katika kiSwahili Asiliya (lahaja ṭisiya za ṁambawo wa ṗani ya Kenya) wazungumzaji wake husema ‘marafiki zangu’ ikawa ‘marafiki’ imo katika ngeli ya JI-MA na mofimu kiwakiliši ča kivumiši ni ča ngeli ya N-N. K̇a mnasaba kuwa ‘vita’ imo katika KI-VI, ambapo tumeoneša sivo katika makala haya, basi yaweza kučukuwa ‘ya’ ambačo ni kihusiši ča ngeli ya N-N k̇a sababu kiSwahili Asiliya čakubali matumizi ya viwakiliši va ngeli mbili katika mfwatano mmoja na likiwa ni neno lililokop̣a.

**Hiṭimišo**

Imewafiki kuwa ‘kita’ nriyo asili ya ‘vita’ lakini si k̇amba yaṭokana na /-ta/ kama alivonena Maalim Abdalla k̇enye makala tuliyonukuu ṭanbihini kuhusu asili ya ‘vita’ au kama alivoṭaja usuli wa ‘vita’ k̇enye makala ya Mkaza. Kinyumewe, učanganuzi wetu umeďihiriša kuwa ni neno lililokop̣a kuṭoka kiPorṭugesi /geha/, k̇ani maPorṭugesi waliṭawala sehemu hizi wakaṭi mmoja na maneno yawo yakaingiya katika kiSwahili. Asili ni /kita/ na kiSwahili kikavumbuwa, k̇a kutumiya kiyasi, wingi wake /vita/ kama ilivofanza k̇enye neno /kiṭabu/ na k̇a wingi /viṭabu/ na /vitamini/ kuṭokuwa na hali ya umoja.

**Marejeleyo**


Abḍalla, A. (2024). Yatokanayo na mkaza (wa)…. Kandi binafsi ya Maalim Abḍilaṭif Abḍalla.

Abḍalla, A. (2017, February 16). Ni "kiasi cha…" sio "kiasi ya…". Kina Wenyewe. https://kinawenyewe.wordpress.com/2017/02/16/ni-kiasi-cha-sio-kiasi-ya/

Mazrui, A. M. (1981). *Acceptability in a planned standard: The case of Swahili in Kenya*. Tasnifu ya Uzamifu (Haijachapishwa). Stanford University, Stanford.

Mlamali, M (1980). *Ikisiri ya Inkishafi*. Longman.

Mulokozi M.M (Mh.) (2012). *Tenzi Tatu za Kale*. TUKI.

Mwalonya, J., Nicolle, A., Nicolle, S. & Zimbu, J. (2004). *Mgombato: Digo-English- Swahili dictionary*. Bible Translation Literacy.

Sacleux, C. S. (1939). *Dictionnaire Swahili-Francais*. Institut d' Ethnologie.

## KIYAMBATIŠO I

| JEḌWALI LA SAMPULI YA ṬAFSIRI ZA NENO "WAR" KATIKA LUĞA ZA KILIMWENGU | | | |
|---|---|---|---|
| **ULAYA** | **TAFSIRI** | **AFRIKA** | **TAFSIRI** |
| Bulgarian | Война /voĭna/ | Arabic | Harb |
| Croatian | Rat/vojna | Somali | Dagaal |
| Czech | Válka | Amharic | T'orineti |
| Danish | Krig | Oromo | Waraana |
| Dutch | Oorlog/krijg | Igbo | Agha |
| English | War | Hausa | Yaki |
| Estonian | Sõda /sota/ | Yoruba | Ogun |
| Finnish | Sota | Kalenjin | Boriet |
| French | Guerre /giigh//lutter | **BANTU** | |
| German | Krieg | Luganda | Olutalo |
| Greek | Pólemos | Kinyarwanda | Intambara |
| Hungarian | Háború/harc | Shona | **Hondo** |
| Irish | Coimhlint ghéar | Xhosa | Imfazwe |
| Italian | Guerra /gerra/ | Zulu | Impi |
| Latvian | Karš /karsh/ | Chewa (Nyanja) | **Nkhondo** |
| Lithuanian | Karas | Sesotho | Ntoa |
| Maltese | Gwerra | Sukuma | Fida |
| Polish | Wojna /voĭna/ | Gikuyu | Kau |
| Portuguese | Guerra (hutamkwa /**geha**/) | Luhya | Olutalo/Eliye |
| Romanian | Război | Kamba | Kau |
| Slovak | Vojna | Gusii | Esegi |
| Slovenian | Vojna | Mijikenra | Viha/kondo |
| Spanish | Guerra /gerra/ | Giriama | Viha cf gwira and Romance Languages |
| Swedish | Krig | Swahili | Vita/k$^{h}$ondo |
| Latin | Bellum | | |
| **ASIA** | **TAFSIRI** | **AMERIKA KUSINI** | **TAFSIRI** |
| Chinese | Zhànzhēng | Quechua | Awqay |
| Hindi | Yuddha | Guarani | Ñorãirõ |
| Indonesian | Perang | Aymara | Ch'axwa |
| Bengali | Yud'dha | | |
| Japanese | Sensō | | |
| Sindhi/Urdu | Janga | | |

**Asili:** https://translate.google.com/?sl=en&tl=de&text=war&op=translate na usaiḍizi wa kiBantu na luğa nyengine za kiKenya kuṭoka wanaCHAKIKA, UoK.

**Kauli Mtakaso:** Maelezo yaliyomo humu ni yangu na si ya UoK wala Iḍara yetu. Kuhusu makala haya, na Elimu ḳa jumla, wasiliyana nami mkarama@kabianga.ac.ke .